Ninafikaje Kituoni?

Kituo kiko sehemu ifuatayo:

5/13-21 Mayes Avenue, Logan Central



Kituo kinafunguliwa lini(siku gani)?

Jumatatu: saa 3 asubuhi – saa 11 jioni
Jumanne: saa 7 mchana - saa 11 jioni
Jumatano: saa 3 asubuhi – saa 11 jioni
Alhamisi: saa 3 asubuhi – saa 11 jioni
Ijumaa: saa 3 asubuhi – saa 11 jioni
Kituo kimefungwa kwenye siku kuu za kitaifa.

Sehemu zingine pakunulizia

Mtandao wa kitaifa wa kutoa msaada juu ya unyanyasaji wa kijinsia unatoa taarifa, rufaa na msaada kwa wanawake nyanyaswa kijinsia wakati wowote wa maisha yao. Mtandao huu wa kusaidia ni:

Simu: 1800 010 120

Huduma juu ya unyanyasaji wa kijinsia katika eneo la Brisbane hutoa msaada wa dharura kwa masaa 24 kwa wanawake ambao wamenyanyaswa kijinsia kwa kipindi kisicho zidi wiki mbili. **Simu: 3636 5206**

Unyanyasaji wa Kijinsia ni nini?

Wanawake wengi na vijana wa kike walipitia unyanyashaji wa kijinsia kwa kipindi cha karibu, kipindi kilichopita na/au utotoni.

Unyanyasaji la kijinsia ni kitendo chochote cha ngonobila hiyali ya mtu.

Hii inaweza kuwa pamoja na kujamiyana bila ridhaa au myenendo ya kulazimisha ngono pamoja na ubakaji.

UNYANYASAJI WA KIJINSIA NI KOSA LA JINAI

Kwa kawaida unyanyasaji wa kijinsia hufanywa na wanaume kwa wanawake na watoto. Ni kosa la jinai la kijinsia.

Mara nyingi, mwaathirika anamujua mharibifu.

Unyanyasaji wa kijinsia siyo kamwe kosa la mwaathirika. Kila wakati mharibifu ndiye anayehusika na unyanyasaji wa kijinsia.

Hakuna msamaha juu ya unyanyashaji wa kijinsia.

Waharibifu katika unyanyasaji wa kijinsia hutumia, cheo, nguvu na uchezeaji wakijaribu kumudu mwili wa mtu mwingine, akili zake na mhemuko wake.

Athari za unyanyasaji wa zinadhuru na mara kwa mara ni za kudumu.

Kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia kinawakaribisha watu wote wanaotokea kwenye nchi zisizoongea lugha ya kingeleza, Aboriginal na Torres Strait Islender, basha(mme anayejamiyana na wanaume), msagaji(mke anayejamiyana na wanawake),watu wenye uke na ume na wenye maumbile ya kimwili yanayowatambulisha tofauti na jinsia yao.

Imefathiliwa na idara ya Afya Queensland(Queensland Health)

Unyanyasaji wa kijinsia siyo kamwe kosa la mwanamke!

Kituo Cha Kupiga Vita Unyanyasaji Wa Kingono

5/13-21 Mayes Ave
Logan Central Q
PO Box 243
Woodridge Q 4114
Phone 07) 3808 3299
Fax 07) 3808 9900
Email admin@casv.org.au
Web www.casv.org.au

Kituo cha Kupiga vita unyanyasaji wa Kijinsia ni nini?

Kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia ni huduma ya kijumuia ambayo imewekwa kwa ajili ya kutoa msaada kwa unyanyasaji wa kijinsia,mahitaji ya mafunzo na taarifa kwa jumuia za Logan, Beenleigh na Beaudesert.

Kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia kimepata tenda la kutoa huduma za usalama na heshima ili kusaidia akina mama na vijana wa kike kwenye mwelekeo wawo wa kupona; kufanya kazi kwa ajili ya kuondoa mira na desturi potovu zinazohusiyana na unyanyasaji wakijinsia ; na kutia moyo jamii kujihusisha na utokomezaji wa unyanyasaji wakijinsia.

Wafanyakazi, menejimenti na wajumbe wote wa kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia wana mpango maalum wa kuondoa unyanyasaji wa kijinsia wakati wa kutoa ushauri nasaha na kuhudumia waathirika wa kosa hili la jinai la kijinsia.

Nani awezaye Kutumia Kituo cha Kupiga vita unyanyasaji wakijinsia?

Kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia huweza kutumiwa na akina mama wote pamoja na vijana wa kike wenye umri wa miaka 12 na kuendelea.Viti vya magurudumu(wheelchair) vinaweza kutumiwa katika kituo hiki.

Kituo cha Kupiga vita unyanyasaji wa Kijinsia Kinatoa huduma gani?

Ushauri nasaha

Ushauri nasaha wa binafsi wa kipindi kifupi na cha wastani unatolewa katika mazingira ya usalama na siri, bila gharama kwa akina mama yeyote, na vijana wa kike wenye umri wa miaka 12 na kuendelea ambao wamekuwa ni waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia kwa muda wa karibu, kipindi cha zamani na/au utotoni.

Ushauri nasaha unatolewa na washauri wenye uzoefu ambao wamepata ufundishaji wa kitaalamu kuhusu unyanyasaji wakijinsia.

Kijana mshauri yupo kwa ajili ya vijana wa kike wenye umri kati ya miaka 12 na 18.

Kazi ya kikundi

Idadi ya vikundi vya kutibu hufanyika katika mwaka na mwezeshaji mwenye uzoefu.

Elimu na mafunzo

Taarifa, elimu na mali vinatolewa kwa jamii. Warsha zinazostahiki na mafunzo vinapatikana kwa mabingwa,vikundi na mashirika waliopo katika maeneo hayo.

Mpango wa mashule nje ya kituo

Ushauri nasaha kwa vijana wa kike wenye umri wa miaka 12 kuendelea pamoja na warsha za kuelimisha kwa vijana hutolewa kwa mashure mengi ya sekondari katika eneo hili.

Taarifa na rufaa

Kituo cha kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia hutoa:

- Taarifa na rufaa kuhusu utaratibu wa kisheria
- Taarifa na rufaa kwa ajili ya afya na mambo ya kiuganga
- Taarifa kwa marafiki na familiya wa akina mama na watoto ambao wamenyanyaswa kijinsia.

Kituo cha Kupiga vita unyanyasaji wa Kijinsia Kinaamini Kwamba waathirika wana haki ya:

- kuaminika
- kusikilizwa na kuungwa mkono
- kutibiwa/kusaidiwa kwa heshima, utu na uelewo
- kutoa habari kwa lugha yao, na mkalimani ikiwa ni lazima
- kupata habari kuhusu chaguo mbalimbali
- kuwa na mamlaka juu ya chaguo lao
- Kutunziwa siri